**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 NA MAONI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2O15/2016

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
**DODOMA**
Mei, 2015.

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 NA MAONI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2O15/2016

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili 2013, niaomba kuwasilishaTaarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 na Maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake ya Kikanuni, katika mwaka wa fedha 2014/15 Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii ilizuru kwa lengo la kukagua utekelezaji wa shughuli zaWizara na taasisi zake ikiwa ni pamoja na kufanya vikao na wahusika.

Pia Kamati ilikagua miradi ya maendeleo katika taasisi hizo ambayo iliidhinishiwa fedha katika mwaka huu wa fedha. Miongoni mwa taasisi zilizotembelewa ni pamoja na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, (NHIF), Taasisi ya Saratani Ocean Road (Ocean Road Cancer Institute), Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Kitengo cha Magonjwa ya Moyo Muhimbili, Kituo cha Mtangamao wa Waathirika wa dawa za Kulevya cha Itega, na Hospitali za Mikoa Morogoro na Dodoma.

Aidha, mwezi April mwaka huu, Kamati ya Huduma za Jamii, ilipata fursa ya kutembelea moja ya Hospitali za Kundi la Apollo iliyopo New Delhi,nchini India, kwa lengo la

kuangalia huduma za tiba ambazo zinatolewa kwa Wagonjwa wa Tanzania wanaopelekwa katika hospitali hizo. Kundi la Hospitali za Apollo lina makubaliano ya kimkataba na Serikali ya Tanzania, yanayowezesha Hospitali hizo kupokea Wagonjwa kutoka Tanzania ambao wanapata rufaa ya kupelekwa nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 01, 04 na 08 Mwezi Mei 2015, Kamati ilifanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Katika kipindi hicho Waziri wa Afya, Dkt. Seif Ali Rashid (Mb) aliwasilisha taarifa kuhusu Fungu 52 – Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na taasisi zilizo chini yake.

**Mheshimiwa Spika,**uwasilishaji wa Mheshimiwa Waziri ulijikita katika maeneo manne Taarifa ya Waziri ilikuwa na maeneo mahususi yafuatayo:

i. Utekelezaji wa maoni ya Kamati yaliyotolewa kwa Wizara katika mwaka wa fedha 2014/2015,

ii. Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2014/15

iii. Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika mwaka wa fedha 2014/2015,

iv. Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na maeneo ya vipaumbele kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015.

**Mheshimiwa Spika**, katika kupitia taarifa ya utekelezaji wa maoni na mapendekezo yaliyotolewa kwa Wizara katika mwaka wa fedha 2014/15 Kamati ilibaini kwamba, kwa sehemu kubwa Wizara imezingatia ushauri uliotolewa jambo ambalo limewezeshwa kupatikana kwa mafanikio yafuatayo:

- Kupungua kwa utegemezi wa fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa kuongeza tengeo la fedha za ndani. Fedha ya maendeleo inayotokana na vyanzo vya ndani imeongezeka kutoka shilingi bilioni 19 katika mwaka wa fedha mwaka 2012/13 hadi kufikia shilingi bilioni 70 katika mwaka 2015/16. Kamati inapongeza hatua hii ya kuweza kuongeza bajeti ya ndani ya maendeleo kwa zaidi ya asilimia 350 ndani ya kipindi cha miaka minne ya bajeti (2012/13 hadi 2015/16) ni imani ya Kamati kwamba iwapo utaratibu huu utaendelea tutapunguza utegemezi wa fedha za wafadhili kwa kiwango kikubwa.

- Kuongezeka kwa ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya taasisi za Wizara kutokana na matumizi ya mfumo wa kielektroniki. Mfumo huu umewezesha baadhi ya taasisi kuvuka lengo la makusanyo. Kwa mfano Hospiali ya Rufaa, Mbeya imeongeza makusanyo kutoka shilingi milioni 50 kwa mwezi hadi shilingi milioni 500.

- Kuongezeka kwa tengeo la fedha za mradi wa huduma ya afya ya Mama na Mtoto kutoka shilingi bilioni 14.5 zilizoombwa hadi kufikia shilingi bilioni 19.5hii ni ishara kwamba Wizara inatambua umuhimu wa eneo hilo kupewa bajeti ya kutosha.

- Kukamilika kwa matengenezo ya mashine 2 za mionzi katika Taasisi ya Saratani ya Oceand road.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya mafanikio hayo bado kuna maeneo yanayokabiliwa na changamoto na hivyo Kamati inashauri yafanyiwe kazi kama ifuatavyo:

i) Fedha za uendeshaji kutolewa pungufu, kucheleweshwa ama kutotolewa kabisa na hivyo kuathiri uendeshaji waHospitali, vyuo vya mafunzo na huduma za ustawi wa jamii.

ii) Ongezeko la idadi ya Wagonjwa wanaopelekwa nje kwa ajili ya matibabu ikilinganishwa na bajeti inayotengwa kwa ajili ya kugharamia matibabu hayo. Hali hii imesababisha deni la matibabu katika Hospitali za Apollo kufikia Dola za Marekani **milioni 9.2** hadi Mwezi wa Machi, 2015.

iii) Bajeti ndogo kwa ajili ya Wahitaji wa Huduma za Ustawi wa Jamii wakiwemo Wazee, Watu wenye Ulemavu na Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.

iv) Kupungua kwa fedha za Wadau wa maendeleo katika sekta ya afya jambo ambalo limeathiri ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo.

v) Fedha ya maendeleo kutoka vyanzo vya ndani kuchelewa au kutolewa kwa kiasi kidogo jambo linaloathiri utekelezaji wa miradi na kusababisha ongezeko la gharama za miradi hiyo, na baadhi ya Wakandarasi kuishitaki Serikali kwa kutowalipa madeni.

vi) Kuendelea kuongezea kwa deni la Serikali kwa Bohari ya Dawa (MSD) ambapo hadi Machi mwaka huu lilikuwa limefikia Sh. **Bilioni 108.6**Hali hii inaiathiri MSD katika kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

vii) Kuboresha huduma za Matibabu ya Saratani nchini na kuiwezesha Hospitali ya Ocean Road kufanya kazi kikamilifu,

iv) Upatikanaji wa Watumishi katika sekta ya afya hususan maeneo ya pembezoni,

v) Huduma za Bima ya Afya kwa wananchi wote,

vi) Utolewaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu nchini ikiwemo wenye ulemavu wa ngozi,

## 3.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2013/2014

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilitengewa jumla ya shilingi **659,743,825,000/=** ambapo kati ya fedha hizo shilingi**354,014,333,000/=**zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (recurrent expenditure) na shilingi **305**, **729**, **492**,**000**/= kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2015Wizara ilikuwa imepokea **shilingi 328,069,157,000/=**sawa na asilimia **58. 4**ya bajeti yote iliyotengwa.Katika kiasi hicho kilichotolewa shilingi **254,345,933,000/**ni kwa ajili ya matumizi ya kawadia, sawa na asilimia **90.9** ya fedha zilizotengwa. Kwa upande mwingine fedha zilizopokelewa katika maendelea ni shilingi

**73,723,224,000** sawa na asilimia **26.1** ya bajeti yote iliyotengwa katika maendeleo.

Katika fedha ya maendeleo iliyopokelewa shilingi **8,800,000,000/=**ni kutoka fedha za ndani ikiwa ni asilimia **16.3** tu ya tengeo la ndani la **shilingi 54,000,000,000/=. Fedha za** nje zilizopokelewa ni**shilingi 73,723,224,000/=** sawa na asilimia **26.8**ya fedha za nje kwenye maendeleo ambazo zilikuwa **shilingi 251,729,492,000/=**

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fedha iliyopokelewa na Wizara hadi Machi, 2015 ilikuwa asilimia 58.4 tu, Kamati inasikitishwa na mwenendo huo wa fedha. Aidha,inahoji ni kwa vipi Hazina itaweza kutoa asilimia 41.6 iliyosalia katika kipindi cha robo iliyosalia kabla ya kumalizika kwa mwaka huu wa fedha wakati imetoa asilimia 58.4 tu ya bajeti ya Wizara katika robo tatu zilizopita.

Mheshimiwa Spika, katika ukusanyaji wa maduhuli hadi Machi, 2015 Wizara ilikuwa imefanikiwa kukusanya shilingi **70,367,588,681** sawa na asilimia 74 ya lengo lake ambalo lilikuwa shilingi **94,585,060,505.** Kiwango hicho cha ukusanyaji ni pungufu kwa asilimia 15 ikilinganishwa na Makusanyo ya kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha uliopita ambayo yalifikia asilimia 89.

## 3.0CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SEKTA YA AFYA NCHINI

**Mheshimiwa Spika,**wakati Kamati ikitathmini utekelezaji wa shughuli za Wizara hii kwa mwaka wa Fedha 2014/2015, ilibaini changamoto kadhaa zinazoikabili sekta ya afya nchini zikiwamo zifuatazo:-

i. Kuendelea kukua kwa Deni la Serikali kwa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ambapo hadi Machi, 2015 lilikuwa shilingi bilioni **108**,

ii. Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuendelea kuwa chini ya kiwango cha asilimia 15 ya bajeti ya Serikali kwa mujibu wa Azimio la Abuja la Mwaka 2001,

iii. Utendaji wa MSD kuhitaji uimarishwe,

iv. Wizara kuendelea kudaiwa na Wakandarasi ambao wanatoa huduma mbalimbali kwa Wizara na Taasisi zake.

v. Wizara kuendelea kutegemea sehemu kubwa ya fedha za maendeleoa (zaidi ya asilimia 82) kutoka vyanzo vya nje.

vi. Ongezeko la Wagonjwa wanaokwenda nje ya nchi kwa ajili ya matibabu ikilinganishwa na bajeti inayotengwa.

vii. Kuendelea kukua kwa deni la Serikali kwa Hospitali za Apollo nchini India ambazo zinapokea wagonjwa wa Tanzania,

viii. Fedha za maendeleo kutotolewa kwa wakati ambapo hadi Machi 2015 Wizara ilikuwa imepokea asilimia 26.1 ya fedha zilizotengwa.

ix. Kusuasua kwa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM),

x. Upungufu wa Watumishi wa sekta ya afya nchini hasa katika maeneo ya vijijini na pembezoni mwa nchi,

xi. Upatikanaji duni wa huduma za Afya ya Mama na Mtoto ikiwemo utoaji wa huduma za uzazi salama na mpango mkakati wa kuzuia vifo vya mama na mtoto.

xii. Kutoeleweka hasa ni kiasi gani kinatengwa kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo,

xiii. Gharama kubwa za matibabu kwa Wagonjwa waSaratani na Figo,

xiv. Bajeti finyu kwa Idara ya Ustawi wa Jamii;

## 4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, imekusudia kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 122,218,398,500 ikiwa ni ongezeko la takribani asilimia 23 ikilinganishwa na malengo ya mwaka wa fedha 2014/15.

Aidha, ili kutekeleza majukumu yake kikamilifuWizara imeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **813,976,870,000/=**ambapo kati ya fedha hizo shilingi **444,618,452,000/=**ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo na shilingi **369,358,418,000**/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, katika kujadili Taarifa ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2015/16 Kamati ilibaini kuwa bajeti ya Wizara imeongezeka kwa takribani shilingi bilioni 191 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2014/15.Kamati inapongeza hatua hii, hata hivyo bado inaishauri Serikali kuendelea kuongeza bajeti ya Sekta ya Afya hadi kufikia lengo la asilimia 15 la bajeti ya taifa kwa mujibu wa Azimio la Abuja, la mwaka 2002.

**Mheshimiwa Spika**, Pia Kamati ilibaini kwamba, Wizara imefanya mapitio ya muundo wake na kuanzisha Idara ya Huduma za Uuguzi na Ukunga (Kifungu 2004) ambayo imetengewa shilingi bilioni 422.3 na Kitengo cha "Huduma za Dawa "Pharmaceutical Services Unit" (Kifungu 2005) ambacho kimetengewa shilingi bilioni 36.6,ili kusimamia na kuboresha huduma za upatikanaji wa dawa katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Ni matumaini ya Kamati kwamba, kuanzishwa kwa maeneo haya mapya ya kibajeti yataleta ufanisi zaidi na kuimarisha huduma katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Kamati inasikitishwa na hatua ya baadhi ya vifungu kupunguziwa fedha katika mwaka ujao wa fedha ikilinganishwa na mwaka uliopita. Vifungu hivyo ni pamoja na 2001 (Huduma za Kinga) ambacho bajeti yake imepungua kutoka shilingi bilioni 275.6 mwaka wa fedha 2014/15 hadi shilingi bilioni 246.3 mwaka ujao wa fedha.

Vingine ni Kifungu 3001 (Idara ya Kinga) ambacho bajeti yake imepungua kutoka shilingi bilioni 34.3 katika mwaka wa fedha 2014/15 hadi shilingi bilioni 33 kwa mwaka wa fedha ujao na , kifungu3002 (Idara ya Uhakiki Ubora wa Huduma za Afya) ambacho bajeti yake imepungua kutoka shilingi bilioni 732.1 katika mwaka wa fedha 2014/15 hadi shilingi bilioni 661.6 kwa mwaka wa fedha 2015/16.

**Mheshimiwa Spika,**Kamati inashauri kwamba, ni vyema Wizara ikahakikisha hatua hiyo haileti madhara kwa maeneo

yaliyoguswa na hatimaye kuathiri utoaji wa huduma za afya nchini.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kujadili makadirio ya bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka 2014/2015, Kamati inatoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

## 5.1 Bajeti ya Sekta ya Afya na Azimio la Abuja

Mheshimiwa Spika,itakumbukwa kwamba, nchi yetu ni miongoni mwa nchi za Afrika ambazo ni Wanachama Wa Umoja wa Afrika, ambazo zimeridhia Azimio la Abuja linalozitaka nchi wanachama kuongeza bajeti katika Sekta ya Afya hadi kufikia asilimia 15 ya bajeti ya Serikali ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, huu ukiwa ni mwaka wa mwisho wa kufikia lengo hilo ni wazi kwamba, hakuna dalili za nchi yetu kufikia kiwango cha asilimia 15 cha bajeti ya Serikali kuelekezwa katika Sekta ya afya. Ushahidi unajionesha kupitia mwenendo wa ongezeko la bajeti ya sekta ya afya katika miaka mitatu iliyopita ambapo ilikuwa asilimia 10.4 kwa miaka ya 2012/13 na 2013/14 na asilimia 10.5 kwa mwaka 2014/15.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Serikali imeshindwa kufikia lengo la Azimio la Abuja katika kipindi hiki cha miaka 10, ni vyema ikajitathmini ili kuona iwapo kushindwa huko kuna athari zozote katika Sekta ya Afya nchini. Aidha, iendelee kutumia Azimio hilo kama lengo la kuendelea kuongeza bajeti ya Sekta ya Afya kwa kadri uwezo wa kiuchumi

utakavyoendelea kuruhusu ili kuboresha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na watumishi katika sekta hiyo.

## 5.2 Upatikanaji wa Dawa, Vifaa tiba na Vitendanishi nchini.

Mheshimiwa Spika, Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ndiyo ina dhamana ya kununua, kuhifadhi na kusambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi kote nchini. Ili MSD iweze kutimiza wajibu huo kikamilifu Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

- Serikali ilipe deni inalodaiwa na MSD (shilingi bilioni 108);

- Serikali itoe fedha ya Ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa mkupuo;

- Taarifa za mapokezi ya dawa kutoka MSD katika Hospitali au vituo vya afya nchini ziweke wazi na Kamati za mapokezi ili kuleta uwazi na ushirikishwaji wa Wananchi;

- MSD ihuishe takwimu za usambazi wa huduma zake mara kwa mara kwa lengo la kujitathmini katika utendaji wake.

## 5.3Bajeti ya Maendeleo na Utegemezi wa Wahisani

**Mheshimiwa Spika**, bado kwa sehemu kubwa shughuli za maendeleo katika sekta hii zinategemea fedha za Wahisani. Kwa Mwaka 2014/2015, jumla ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni sh. **305,729,492,000/=** ambapo fedha kutoka vyanzo vya ndani ni shilingi **54,000,000,000/=** na

fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo ni shilingi **251,729,492,000/** sawa na asilimia **82.3**

Mwenendo huo ndiyo unaojitokeza pia katika mwaka ujao wa fedha, ambapo asilimia 84.2 ya bajeti yote ya maendeleo inategemea fedha za nje. Ni wazi kwamba, utekelezaji wa miradi utaendelea kuathirika kwani fedha hizo za Wahisani zimekuwa hazitolewi kwa wakati na kutolewa kwa kiwango kidogo. Pia wakati mwingine miradi imekwama kabisa baada ya Wahisani hao kujitoa katika ufadhili.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Serikali kuongeza nguvu katika kuimarisha vyanzo vya mapato vya ndani ili viweze kutumika katika ya miradi ya maendeleo.

**5.4Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 201/2015**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kutembelea miradi ya maendeleo ukiwemo ujenzi wa jengo la tiba na wodi ya Wagonjwa katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Taasisi ya Saratani Ocean Road, Hospitali ya Magonjwa wa Akili Mirembe, na Kitengo cha Tiba ya Moyo Muhimbili, inashauri mambo yafuatayo:

i) Ili jengo jipya la MOI lianze kutumika, Serikali iwezeshe upatikanaji wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya ununuzi wa mitambo na vifaa tiba kiasi cha shilingi bilioni 12.5. Aidha, shilingi bilioni 1.8 zilizotengwa kwa ajili ya kuanza kulipia deni la ujenzi kutoka Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) zitolewe ili kutoathiri mwenendo wa kifedha wa mfuko huo.

ii) Fedha za ukarabati wa miundombinu na ununuzi wa vifaa tiba katika Taasisi ya Saratani Ocean Road, kiasi cha shilingi bilioni 14 zitolewe kwa wakati ili

kuhakikisha miundombinu husika inakuwa katika hali nzuri kwa lengo la kutoathiri utoaji huduma kwa Wagonjwa wa Saratani.

iii) Kwa upande wa Hospitali ya Mirembe, Serikali ihakikishe shilingi bilioni 124 zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika kituo cha Waathrika wa dawa za kulevya zinatolewa ili kuepusha matukio ya wagonjwa hao kutoroka na kufanyia fujo wagonjwa wa matatizo mengine pamoja na wafanyakazi.

iv) Kamati inapongeza hatua ya kuanza kazi kwa kitengo cha tiba ya magonjwa ya Moyo Muhimbili, na inashauri Serikali kukiwezesha kwa raslimali fedha na watu ili kifanye kazi kwa ufanisi na kusaidia Watanzania na pia kupunguza hitaji la huduma hiyo nje ya nchi.

## 5.5Maduhuli ya Serikali katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba, zipo taasisi za Wizara ambazo zimeonesha mafanikio katika eneo la ukusanyaji na udhibiti wa maduhuli kutokana na kuanza kutumia mfumo wa kielektoniki. Mfano ni Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya ambayo imeongeza mapato kutoka shilingi milioni 50 hadi 500 kwa mwezi. Aidha, Kamati inaipongeza sana Hospitali hiyo.

Kamati inashauri Wizara kuhakikisha taasisi zake zinaingia katika matumizi ya mfumo huu wa kielektroniki ili kuongeza uwezo wa kukusanya na kudhibiti mapato.

## 5.6Huduma ya Afya ya Mama na Mtoto

**Mheshimiwa Spika**, uhakika wa huduma bora ya afya kwa Mama na Mtoto ndiyo msingi wa ustawi wa jamii na ndiyo kipimo cha utoaji wa huduma ya afya katika jamii. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza bajeti katika eneo hili ambapo katika mwaka uliopita Wizara iliongeza bajeti katika eneo hili kutoka shilingi bilioni 14.5 hadi bilioni 19.5.

Aidha, Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa majengo ya upasuaji katika mkoa wa Tabora (Hospitali ya Rufaa ya Mkoa – Kitete, na Hospitali za Igunga na Nzega) na mkoa wa Mara (Hospitali ya Serengeti).

Kamati inashauri Serikali iendelee kuboresha eneo hili kwa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi nchini kwa kuongeza utoaji wa chanjo, dawa za uzazi wa mpango, upatikanaji wa vifaa vya kujifungulia na motisha kwa watumishi wa sekta ya afya.

### 5.7 Mpango wa Bima ya Afya kwa wote

**Mheshimiwa Spika**, afya nzuri na ya uhakika ni jambo la kwanza la msingi kwa binadamu yoyote. Hilo pia ndiyo hitaji kwa Watanzania na ndiyo maana Kamati imekuwa ikisisitiza juu ya utaratibu wa bima ambao utahusisha makundi yote katika jamii. Pamoja na kuipongeza Serikali kwa azma ya kuwezesha mpango huu Kamati inashauri yafuatayo:-

- Kukamilisha Mkakati wa Ugharamiaji wa Afya (Health Care Financing Strategy) utakaotoa mfumo mzuri wa ugharamiaji wa huduma ya afya;
- Kutoa Mwongozo wa kujiunga na mfumo wa Bima ya Afya utakawezesha kupata huduma bila kikwazo cha gharama (Universal Coverage).
- Elimu ya kutosha itolewe kwa jamii ili iweze kuunga mkono mpango huu

## 5.8 Idara ya Ustawi wa Jamii

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Ustawi wa Jamii ni suala mtambuka linalogusa makundi tofauti katika jamii, Kamati imekuwa ikishauri Idara hii kuweka chini ya mamlaka inayoshughulikia masuala mtambuka, Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ina jukumu la kuratibu shughuli za Wizara zote. Hata hivyo, kumekuwa na hali ya kusuasua katika kutekeleza ushauri huo. Kamati inaendelea kusisitiza yafuatayo:

- Huduma za Idara hiyo ziendelee kuboreshwa kwa kutengewa bajeti kubwa ili kuwezesha makundi ye mahitaji maalum katika jamii kupata huduma stahiki.

- Wizara kupitia Idara hii iendelee kuhamasisha jamii kuandaa miundombinu rafiki kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum ili kuwawezesha kupata huduma na kutekeleza shughuli zao bila vikwazo.
- Serikali iendelee kuboresha vituo vya Ustawi wa Jamii ikiwa ni pamoja na vituo vya watoto yatima, walemavu, makazi ya wazee na mahabusu ya watoto ili kuwawezesha kuishi katika mazingira mazuri.

## 5.9 Huduma kwa Watu wenye Ulemavu wa Ngozi

Mheshimiwa Spika, ni wazi ukatili na mauaji ya ndugu zetu wenye ulemavu wa ngozi “Alibnism” yamekuwa janga linaloisumbua nchi yetu na kuharibu jina zuri la Tanzania. Kamati inaungana na jamii nyingine kulaani na kukemea uendekezaji wa mila potofu za kutafuta mafanikio kwa kutumia viungo vya wenzetu hawa. Aidha wenzetu hawa wanahitaji kuthaminiwa na kupata huduma stahiki kama

makundi mengine katika jamii. Kwa mantiki hiyo Kamati inashauri yafuatayo:

- Kesi za Watuhumiwa wa mauaji na ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi, zipewe kipaumbele na vyombo vya sheria na hatua kali zichukuliwe dhidi ya watakaotiwa hatiani.

- Serikali kupitia Wizara ya Fedha iangalie uwezekano wa kutoa msamaha wa kodi kwa malighafi na vifungashio vya mafuta ya kulainishia ngozikwa watu wenye albinism ili kuzuia mionzi ya jua (Sun Skin Cream)ili bidhaa hiyo izalishwe kwa wingi hapa nchini na kwa gharama nafuu.

- Kuwe na mkakati maalum wa kutoa elimu kwa jamii dhidi ya imani potofu kwamba wanaweza kufanikiwa katika maisha kwa kutumia viungo vya watu wenye albinism.

## 5.10 Sheria ya Madaktari ya Mwaka 1959 *(The Medical and Dental Practitional Act, 1959)*

**Mheshimiwa Spika,** katika Bunge la bajeti lililopita Kamati ilishauri Serikali kuwasilishwa Muswada waSheria ya Madaktari na Madaktari wa Meno kwani iliyopo ni ya muda mrefu sana (1959).

Muswada huo ni muhimu kwani tasnia ya udaktari nchini imekuwa ikipitia mabadiliko mbalimbali ambayo yanahitajika kujumuishwa katika taaluma ya Tiba. Kamati inaishauri Serikali kukamlisha Muswada huo wa Sheria na kuuwasilisha Bungeni ili kupata Sheria ambayo itawezesha Madaktari kutekeleza majukumu yao kikamilifu na kwa weledi.

## 5.11Huduma ya Tiba ya Saratani nchini

**Mheshimiwa Spika**, tatizo la Saratani limeendelea kuongezeka nchini ambapo Wagonjwa wengi wamekuwa wakipokelewa na kupatiwa matibabu katika Taasisi ya Saratani Ocean Road. Hata hivyo matibabu hayo yamekuwa ya gharama kubwa kiasi cha kuwafanya watu wa kipato cha chini washindwe kumudu. Kamati inashauri mambo yafuatayo:

- Serikali iongeze ruzuku yake kwa taasisi hii ili kuiwezesha iendelee kutoa huduma kwa gharama nafuu kwa Wagonjwa wa Saratani,

- Serikali ianzishe vituo katika Hospitali za Kanda kama vile, Bugando, KCMC, Hospitali ya Rufaa ya Mbeya, na kadhalika ili viweze kutoa huduma za awali kwa Wananchi wa mikoani kabla hawajalazimika kuja Ocean Road,

- Serikali iangalie namna ya kutumia teknolojia ya wa Tele - Medicine kwa kushirikiana na Hospitali za nchini India ambazo ziko tayari kwa ushirikiano huo. Utaratibu huo utasaidia Wagonjwa wa Saratani nchini kupata huduma ya Madaktari Bingwa kutoka nchini India bila kulazimika kwenda huko,

- Serikali ihakikishe inatoa fedha za kutosha ili kuhakikisha ukarabati wa Mashine za mionzi katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*muda wote.

## 5.12 Uanzishwaji wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika**, ili Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu (GCLA) uweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu unahitaji kuwa na sheria ya uanzishwaji wa Maabara yake. Mchakato wa Muswada huo ulienda sambamba na ule wa Wataaluma

wa Kemia, lakini umeshindwa kukamilishwa katika Mikutano Miwili ya Bunge iliyopita. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha Miswada hiyo inakamilika kabla ya kumalizika kwa Muda wa Uhai wa Bunge hili ili kuwezesha chombo hicho kutekeleza majukumu yake kikamilifu ikiwa ni pamoja na kutunza Kanzi data (data base) ya Vinasaba vya Binadamu (DNA).

## 5.13 Upungufu wa Watumishi wa Sekta ya Afya katika maeneo ya pembezoni

Mheshimiwa Spika, ni wazi maeneo ya pembezoni katika nchi yetu yanakabiliwa na uhaba wa Watumishi wakiwemo wa Sekta ya Afya, ili kupunguza uhaba wa Watumishi wa Sekta ya Afya katika maeneo hayo Kamati inashauri yafuatayo:-

- Serikali iandae mkakati maalum wa kupata Watumisi walio tayari kufanya kazi katika maeneo hayo;

- Serikali iangalie uwezekano wa kusomesha vijana kutoka maeneo husika na kuingia nao mkataba wa utumishi mara wanapohitimu;

- Kuingia mkataba na wahitimu wa Sekta ya Afya wa kufanya kazi maeneo ya pembezoni kwa kipindi maalum kabla ya kuhama. Mkataba unaweza kuhusisha pia posho maalum kwa watumishi hao.

## 5.14 Deni la Matibabu nchini India

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea moja ya Hospitali za Apollo nchini India, iligundua kwamba, deni inalodaiwa Serikali yetu kutokana na gharama za matibabu ya Watanzania katika hospitali hizo limefikia takribani dola za Marekani milioni 9. Kamati inashauri Serikali kuweka utaratibu wa kulipa deni hilo ili kutokiuka mkataba wa makubaliano baina ya Serikali na Hospitali za Apollo wa kuwadumia Wagonjwa wa Tanzania.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, ninapenda kukushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Taarifa ya Kamati.Nikushukuru pia namna ambavyo umekuwa tayari kutoa ushauri na maelekezo kwa Kamati pale tulipokuhitaji.

**Mheshimiwa Spika**, pia niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za jamii kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati, na hasa wakati wa kuandaa taarifa hii. Niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Stephen Hillary Ngonyani, Mb - M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Fatuma Abdallah Mikidadi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Agripina Zaituni Buyogera, Mb - "
5. Mhe. Faki Haji Makame, Mb - "
6. Mhe. Christowaja Gerson Mtinda, Mb - "
7. Mhe. Riziki Omar Juma, Mb - "
8. Mhe. Ezekia Dibogo Wenje, Mb - "
9. Mhe. Antony Gervas Mbassa, Mb - "
10. Mhe. Ali Juma Haji, Mb - "
11. Mhe. Juma Sururu Juma, Mb - "
12. Mhe. Gregory George Teu, Mb - "
13. Mhe. Abia Muhama Nyabakari, Mb - "
14. Mhe. Salome Daudi Mwambu, Mb - "
15. Mhe. Zabein Muhaji Mhita, Mb - "
16. Mhe. Mohamed Gulam Dewji, Mb - "
17. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb - "
18. Mhe. Prof. Kulikoyela K. Kahigi, Mb - "
19. Mhe. Asnain Muhamed Murji, Mb - "
20. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb - "
21. Mhe. Abdulaziz Muhamed Abood, Mb - "

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati ninawapongeza Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Dkt. Seif Suleiman Rashid (Mb), na Naibu Waziri Dk. Kebwe Steven Kebwe (Mb) kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati katika

kipindi chote hiki. Aidha, ninampongeza Katibu Mkuu Dkt. Donald Mbandona Wataalam wote wa Wizara, kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili na kuchambua bajeti ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla. Pia niwanawashukuru Makatibu wa Kamati Ndugu Chacha Nyakega na Ndugu Happyness Ndalu, wakisaidiwa na Ndugu Jane Ndulesi,kwa kuratibu shughuli za Kamati na kuandaa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, **Fungu 52,** jumla ya **shilingi 813,976,870,000/=** kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika,**baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja hii na ninaomba kuwasilisha.

**Marrareth Simwanza Sitta, (Mb)**
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII**
02 Juni, 2014